(١)

Majukumu

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:{Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Na baada ya utangulizi huu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemkirimu mwanadamu na akamuumba kwa kumpa mikono miwili na akampulizia roho yake na akawafanya malaika wamsujudie na akamfanya kuwa bora kwa mambo mengi kuliko viumbe vyake vingi. Na miongoni mwa mambo hayo ni uwezo wake wa kubeba majukumu na utekelezaji wa majukumu ya kisheria. Kwa hiyo Mtu mwenye akili timamu hawezi kujivua majukumu bila kujali nafasi yake katika jamii. Kila mtu ana jukumu kwa mujibu wa uwezo alionao na jinsi anavyoweza kuhimili kazi anazopewa. Na jambo ambalo halina shaka ni kuwa majukumu ni dhamana kabla ya kuwa utukufu, na yoyote atayeyaangalia majukumu kwa lengo la utukufu peke yake huku akiwa na shauku ya kuyapata kwa ajili ya kuitukuza nafsi yake, mara nyingi hutelezeshwa na mabaya yake na matokeo yake, na mwenye kuyachukua majukumu kwa haki yake na kuyachukulia kama ni Ujumbe basi mtu huyu

kwenye majukumu yake ana usaidizi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: na Katika hili, Mtume wetu Muhammad anasema S.A.W: akimwambia Abu Rahman bin Samrah: Ewe mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu usiombe isipokuwa mara moja. Hakika Wewe utakapopewa bila ya kuomba utakuwa umesaidiwa na ikiwa utapewa kwa kuomba utakuwa umepewa uwakilishi wa hicho ulichokiomba.

Na kutoka kwa Abuu Dhari R.A, amesema: nilisema: Ewe Mtume wetu S.A.W: je unaweza kunitumia mimi? Na Mtume S.A.Wakaupiga mkono wake katika bega lake kisha akasema: Ewe Abuu Dhari hakika Wewe ni mnyonge wa mwili, na hii ni dhamana, na hakika hii siku ya Malipo ni ya kufedhehesha na kuleta majuto isipokuwa kwa yule atakaye ichukua kwa haki yake na akatekeleza jukumu lake.

Na majukumu yana sura nyingi: Kuna majukumu ya familia, Hakika familia ina Mchango mkubwa katika kuleta utulivu wa jamii na mshikamano wake. Kwani hiyo ni nguzo imara katika ujenzi wa ngome ya ulinzi ya Kwanza ya familia. Na wazazi wawili wana majukumu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kuijenga familia na kuleta utulivu wake kupitia majukumu ya kila mmoja wao na kutekeleza dhamana ya haki za wengine.

Uislamu umeweka wazi majukumu haya na hizo haki na kuyagawa baina ya kila mwana familia ambapo anasema Mtume S.A.W: Nyinyi wote ni wachunga, na kila mmoja wenu ataulizwa aliowachunga. Mwanaume ni mchunga wa watu wake na ataulizwa kwa anaowachunga. Na mwanamke ni mchunga katika nyumba ya mume wake na ataulizwa kwa anaowachunga. Na mtumishi ni mchunga wa mali ya mkuu wake na ataulizwa kwa alichokichunga. Na kwa hivyo nyinyi nyote ni wachunga na nyote

mtaulizwa mnachokichunga. Kwa hiyo, mafanikio ya familia na utulivu wake vinategemea ulinzi wa haki na uwajibikaji wa kila mtu miongoni mwa wanafamilia, na kutoyapuuzia hayo yote au kupindukia ndani yake. Kwa hiyo majukumu ya kila mmoja katika familia ni ya kiushirikiano: Haki, wajibu, na kuheshimiana, kwamba kila mmoja autekeleze wajibu wake kwa upendo na mapenzi na uaminifu, na kwa yule atakaye puuzia au kuchupa mipaka au alipoteza jukumu lake basi atambue kwamba yeye ana maswali ya kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Je alililinda au alilipoteza jukumu hilo? Anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni atamuuliza kila mtu kwa kile alichokilinda, je alikihifadhi au alikipoteza, mpaka atamuuliza mtu kuhusu watu wake wa nyumbani. Na anasema Mtume S.A.W: Inamtosha mtu kupata madhambi kwa kupoteza haki za anaowalea.

Na miongoni mwa aina za majukumu: Ni majukumu ya kikazi: ambapo jambo hili linakuwa kubwa kwa ukubwa wa kazi ya mtu aliyopewa aifanye. Kwa hiyo kila wigo wa majukumu unapoongezeka huhitajika mambo maalumu. Na muhimu zaidi kati ya Mambo hayo ni: kuwa na uwezo wa kutosha, kutosheka, uzoefu, Uaminifu, uwezo wa kufanya kazi na yanayoambatana nayo, kwa namna ambayo kila mtu anaweza kubeba jukumu lake mbele yake na mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa yale aliyompa uongozi ambapo Mtume S.A.W anasema: Hakuna mtu yeyote anaewaongoza watu kumi au zaidi ya watu kumi isipokuwa ataenda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huku mikono yake ikiwa imefungika shingoni mwake (kwa maana ya kubeba jukumu) na kitakachoiondoa mikono yake hiyo ni Wema wake au uovu wake ukaendeza hali hiyo. Kama ambavyo kila mtu anaewaongoza watu au katika kazi anapaswa atambue kwamba yeye ni mwenye kuamrishwa kufanya kazi yake kama itakiwavyo, na kumwogopa mwenyezi Mungu Mtukufu, na anapaswa atambue

kwamba yeye ni msimamizi wa mali ya uma, na kwa ajili hiyo atafanya kazi kwa mujibu wa mipaka yake ya kiutendaji na ya kikazi. Anatakiwa asijiingize katika katika vinavyomchukiza Mwenyezi Mungu Mtukufu au vya Haramu kwa jina lolote liwalo miongoni mwa majina mbali mbali.

Na kwamba sisi tunasisitiza sana kuwa jukumu lolote na ngazi yoyote haipaswi na wala haiswihi pawepo na uzembe tegemezi au kutofuata maelezo ya kina ya kazi zote zilizo chini ya jukumu la mtu, vyovyote lionekanavyo dogo kwa mtu huyo au jepesi, kwani katika yale wanayoyadhania wwtu kuwa ni madogo au mepesi, uzembe wa kuyatekeleza unaweza ukapelekea madhara yasiyotegemewa, na sisi sote tunalazimika kutambua kwamba kujiamini hakumaanishi kutofuatilia na kwamba ufuatiliaji haumaanishi ukosefu wa kujiamini. Vile vile kila mtu mwenye majukumu kwa mujibu wa nafasi yake ya majukumu, anatakiwa achague wasaidizi wake wenye nguvu na waaminifu na achague wenye kufaa zaidi, na yoyote atakaye mpa jukumu la kazi mtu katika watu wakati katika wao kuna aliye bora zaidi - kwa maana zote za ubora zinazofaa - kwa kazi hiyo kuliko aliyelepewa, basi atakuwa amemfanyia hiana Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake S.A.W, na atakuwa mhaini wa nchi pamoja na amana aliyopewa aibebe.

Na miongoni mwa aina za majukumu ya kijamii: Uislamu umeweka udhibiti wa kijamii ambapo watu wanaishi maisha ya usalama na utulivu kupitia udhibiti huo, huku upendo, na heshima, kuleana na kushikamana kijamii vikitangaa kwa msingi wa usawa baina ya watu wote, na jamii hiyo ikawa mfano wa mwili mmoja.

Na mwenye kuuzingatia uhalisia wa watu hii leo, atakuta miongoni mwao kuna fakiri ambae hana cha kumwondoshea njaa yake na mgonjwa asiyeweza kupata dawa, na wanawake waliofiwa na waume zao, na mayatima walio wanyonge, na watu wasiokuwa na watoto.

Na kuwasaidia mahitaji yao watu hawa ni katika majukumu ya kijamii na ya kisheria na ya kitaifa bali majukumu haya ni katika faradhi za kutoshelezeana ambazo wanapotekeleza baadhi basi jukumu hilo huondoka kwa wengine, na kama hakuna yoyote anayelitekeleza basi watu wote hupata madhambi makubwa. Na kwa ajili hiyo, anasema Mtume S.A.W: Hatakuwa ni mwenye kuniakini mimi yule atakayelala hali ya kuwa ameshiba na jirani yake wa nyumba ya pili ana njaa na yeye anajua hivyo.

Mtume S.A.W amelipa cheo kikubwa Suala la kubeba majukumu ya kijamii na akajaalia kukidhi mahitaji ya watu kunatangulizwa mbele ya Ibada ya Itikafu katika msikiti wake wa Madina. Na kutoka kwa Abuu Sa'ad l hudhriy R.A, anasema: Tulipokuwa safarini na Mtume S.A.W, alikuja mtu mmoja akiwa juu ya kipando chake akawa anatazama kulia na kushoto, na Mtume S.A.W akasema: Mtu yeyote mwenye kipando cha ziada basi na ampatie yule asiye nacho. Na yoyote mwenye chakula cha ziada basi na ampatie yule asiye nacho. Na kisha akasema S.A.W: Mtu anayependwa zaidi na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni yule mwenye kuwanufaisha watu zaidi. Na Katika Mambo mazuri mno kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni furaha unayoiingiza katika moyo wa muislamu, au ukamwondoshea jambo zito au kumlipia Deni lake au kumwondoshea njaa. Na mimi kutembea na Ndugu yangu mwenye shida ni bora zaidi kwangu kuliko kukaa itikafu Mwezi mzima katika Msikiti wangu huu - kwa maana ya Msikiti wa Madini - na yoyote atakayeenda na nduguye mwenye shida mpaka akamsaidia basi Mwenyezi Mungu Mtukufu atamtia nguvu katika mguu wake Siku ambayo miguu itakwenda kombo.

Na Mtume S.A.W alikuwa na ari ya kuwafuatilia Maswahaba wake katika kuwasaidia watu mahitaji yao na kuyashughulikia masilahi yao, na akawa akimuuliza aliyefanya Jambo na aliyeitikia wito wake na yule aliyepupia na kuufuata mwongozo wake, akasema siku moja S.A.W: Ni nani miongoni mwenu leo ameamka akiwa amefunga? Akasema Abuu Bakar R.A, Mimi. Akasema Mtume S.A.W: Na ni nani

miongoni mwenu aliyesindika jeneza leo? Abuu Bakar akasema: Mimi. Kisha Mtume akasema: Ni nani miongoni mwenu aliyemlisha masikini leo? Abuu Bakari akasema: Mimi. Mtume S.A.W akasema: Na ni nani miongoni mwenu aliyemtembelea mgonjwa leo? Abuu Bakari akasema: Mimi. Mtume S.A.W akasema: hayakusanyiki Mambo haya yote kwa mtu yeyote isipokuwa Mtu huyo ataingia Peponi.

Na miongoni mwa aina za majukumu: Ni majukumu ya kitaifa: Kwani hakika nchi ina haki zake kwetu sisi sote na sisi tuna jukumu kubwa kwa nchi, ili tuilinde na kufanya kazi ya kuinyanyua na kuipeleka mbele. Na Mtume S.A.W aliwalea na kuwafunza Maswahaba wake R.A, kwamba kujitolea nafsi na mali kwa ajili ya kulinda nchi na vitu vyake viheshimiwe na vitakatifu vyake ni jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; na hakuna chenye kuleta maana ya hayo kuliko yeye mwenyewe Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyekwishanyanyua cheo cha wale waliojitolea roho zao kwa ajili ya kuilinda Dini yao au nchi zao.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ}.

{Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani}

Na vile vile, miongoni mwao majukumu ya kitaifa ni kufanya kazi ya Ujenzi wa taifa, na kulinyanyua juu, kwa kuyatanguliza masilahi makuu ya nchi juu ya masilahi yake binafsi, na kuunganisha juhudi pamoja na kupiga vita tofauti, na kutoϒtenganisha muungano na

wote kuwa kitu kimoja kwa ajili ya kutekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا}،

{Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَلَا تَنَازَعُوا فَتَفْشَلُوا وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ وَاصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ} .

{...wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri}

Na sisi tunatakiwa kutambua kuwa itatujia siku ambayo watu wote wataambiwa:

{وَقِفُوهُمْ إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ}

{Na wasimamisheni. Hakika hao wataulizwa}

Na kwa pamoja tuyahisi maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

{يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنكُمْ خَافِيَةٌ} ،

{Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yoyote yenu}

Bila kujali ukubwa au udogo wa kitu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{إِنَّهَا إِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِنْ خَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَاوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ يَأْتِ بِهَا اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ}.

{... Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo fichika, Mwenye khabari za yote}.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya wa Mwisho katika Mitume, na Wajumbe wake, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayemfuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.
Mlango.

Ndugu zangu Waislamu

Baada ya masaa machache tutaukaribisha msimu wa Kheri na baraka na utiifu, ambao ni mwezi wa Shaabani uliobarikiwa, mwezi ambao Matendo ya waja hunyanyuliwa ili yawekwe mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa hiyo Mtume S.A.W alikuwa akiuhusisha na Ibada nyingi na utiifu kwa Mola wake, na kujikurubisha kwake, kwa ajili hiyo,Mtume S.A.W alikuwa akiongeza ibada ya kufunga kwa kiasi ambacho Maswahaba wake R.A, walimuona mpaka baadhi yao wakamuuliza siri ya kuupa umuhimu mkubwa mwezi huu wa Shaabani. Na kutoka kwa Usama bin Zaid R.A, anasema: nilisema kumwambia Mtume S.A.W: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu

Mtukufu, sijawahi kukuona mimi ukifunga mwezi wowote kama unavyofunga katika mwezi huu wa Shaabani. Akasema: Huo ni mwezi ambao Watu huusahau kwa kuwa kwake baina ya mwezi wa Rajabu na mwezi wa Ramadhan, na huu ni mwezi ambao Matendo ya waja hunyanyuliwa na kupelekwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, na mimi ninapenda matendo yangu yanyanyuliwe na kupelekwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huku nikiwa nimefunga.

Na kutoka kwa Bi Aisha, Mama wa waumini R.A, anasema: Mtume S.A.W, alikuwa anafunga mpaka tukawa tunasema: hafungui kinywa, na alikuwa akifungua kinywa mpaka tukawa tunasema: hafungi. Na sijawahi kumuona Mtume S.A.W, akifunga na kuikamilisha mwezi isipokuwa Mfungo wa Mwezi wa Ramadhani, na sijawahi kumuona akifunga kwa wingi kuliko afanyavyo katika mwezi wa Shaabani.

Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameufanya mwezi huu wa shaabani uwe na usiku uliobarikiwa ambapo yeye huwaangalia waja wake kwa jicho la huruma na upole, na kuwasamehe kwa fadhila zake makosa yao pamoja na kuzisitiri aibu zao. Na usiku huo si mwingine bali ni ule wa nusu ya mwezi wa Shaaban. Na kutoka kwa Abuu Musa Ash-ariyi R.A, anasema: kwamba Mtume S.A.W amesema: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huchomoza katika usiku wa nusu ya mwezi wa Shaaban na wasamehe waja wake wote isipokuwa mshirikina au mgomvi wa kupindukia. Na katika mapokezi mengine: Mwenyezi Mungu huwachomozea waja wake usiku wa nusu ya mwezi wa Shaabani na kisha akawasamehe Waumini wote na anawapa muda makafiri na kuwaacha watu wa chuki na chuki zao mpaka atakapowaita.

‘

Sisi tunapaswa kuyatumia masiku haya yaliyobarikiwa kwa kukithirisha Ibada ya utiifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujikurubisha kwake Mola Mitukufu kama utekelezaji wa kauli ya Mtume S.A.W: Hakika ana Mola wenu katika masiku haya mazuri ya kuwapa waja wake, basi jisogezeni katika hayo huwenda mmoja wenu atakayepatwa na moja kati ya mazuri hayo hatatenda uovu milele baada yake

(١٠)

Ewe Mola wetu tunakuomba utusaidie tuwe ni wenye kukukumbuka na kukushukuru na tukawa waja wako wema.